

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO



MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI

23 JUNI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA HAMSINI – TAREHE 23 JUNI, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**439. MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA
(UKONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali itatenga siku za kutoa huduma Ofisi za Dar es Salaam ili kupunguza gharama kwa wanaosafiri kufuata huduma Dodoma.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**440. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA
(NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-


Je, ni lini Serikali itatenga fedha kununua vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Mtakanini – Namtumbo.

WIZARA YA MADINI:

441. MHESHIMIWA NORAH WAZIRI MZERU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wachimbaji wadogo wa Madini wa Ulanga kupata masoko ya uhakika.



WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

442. MHESHIMIWA MWANTUM MZAMILU ZODO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni lini Serikali itajenga Soko la kisasa la Wavuvi katika Ukanda wa Pwani.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

443. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, kuna mkakati gani wa kuwanusuru Vijana wanaoshiriki Mchezo wa Kamari kwa matarajio ya kupata fedha ya haraka.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

444. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-


Je, ni lini Wananchi wa Kata ya Mbasa na Katindiuka watalipwa fidia kwa kupisha ujenzi wa barabara inayoelekea Malinyi na Ulanga.

III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2022 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2022*); na

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2022 (*The Water Resources Management (Amendment) Bill, 2022*).



IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali Kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2021 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Kwamba, Bunge sasa likubali Kupokea na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
23 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, ndc
KATIBU WA BUNGE**

